**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA KIGOMA**
**MTIHANI WA UTIMILIFU MKOA (MOCK) KIDATO CHA NNE**

**02** **KISWAHILI**

**MUDA: SAA 3:00** **$15^{TH}$ JULY, 2025 2:00 PM**

---

## MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali **kumi na moja(11).**
2. Jibu maswali yote katika sehemu **A** na **B**, na maswali mawili (2) kutoka sehemu **C** ambapo swali la **tisa** (9) ni la lazima.
3. **Sehemu A**ina alama **kumi na sita (6)**, **sehemu B** alama **hamsini na nne (54)** na **sehemu C** ina alama **thelathini (30)**.
4. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa **bluu au mweusi**.
6. Vifaa vya mawasiliano na vitu visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
7. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



Scanned with CamScanner

**SEHEMU A (alama 16)** Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Katika kipengele( i) hadi (x) chagua herufi ya jibu sahihi kasha andika herufi ya jibu hilo kwenye kijitabu chako cha kujibia.

i. Ni jambo gani linalodhihirihisha umbo la nje la kazi ya fasihi?
   A. Muundo
   B. Jina la kitabu
   C. Fani
   D. Mtindo
   E. Maudhui

ii. Anatoa ufafanuzi juu ya ubantu wa Kiswahili kwa kueleza wakazi wa mwambao waliojulikana kama"Wazanji" na watawala wao walijukana kama " Wakilimi".
   A. ALi-Idris
   B. Al-Masudi
   C. Marco Polo
   D. Ibin Batuta
   E. Fumo Liyongo

iii. Maria alinunua vitabu vizuri Vizuri vyote viliwekwa kabatini. Dada alivipanga vizuri. Katika mfuatano wa sentensi hilo neno vizuri limetumika kama?
   A. Kiwakilishi, kivumishi na kielezi
   B. Kivumishi, kielezi na kiwakilishi
   C. Kiwakilishi, kielezi na kivumishi
   D. Kivumishi, kiwakilishi na kielezi
   E. Kielezi, kivumishi na kiwakilishi

iv. Ni sentensi ipi sahihi zaidi kuhusu viambishi?
   A. Viambishi vyote ni mofimu
   B. Viambishi vyote hutokea baada ya mzizi
   C. Viambishi vyote ni maneno yanayowekwa katika mzizi wa neno
   D. Viambishi vyote ni mofimu tegemezi isipokuwa mzizi wa neno
   E. Viambishi vyote vinakamilisha maana

v. Ipi ni seti sahihi ya vipera vya semi?
   A. Methali, mizungu na maghani
   B. Soga, nyimbo na nahau
   C. Misemo, mafumbo na vigano
   D. Mafumbo, soga na maghani
   E. Nahau, vitendawili na mizungu

vi. Ni aina ya wahusika ambao hawabadiliki na wamepewa majina ambayo humfanya msomaji aelewe tabia na matendo yao.
   A. Wahusika duara
   B. Wahusika bapa sugu
   C. Wahusika wakuu
   D. Wahusika bapa vielelezo
   E. Wahusika shinda

vii. Mofimu KU iliyopigiwa mstari imebeba dhima gani katika kitenzi siku<u>ku</u>kumbuka.
   A. Ukanushi wakati uliopita
   B. Ukanushi nafsi ya kwanza umoja
   C. Kauli ya kutendeka
   D. Kiambishi kirejeshi
   E. Kudokeza mtendwa

viii. ………………… mna watu wengi.
   A. Aliingia
   B. Alimoingia



Scanned with CamScanner

C. Alikoingia
D. Alivyoingia
E. Alipoingia

ix. Sababu ipi kati ya hizi zifuatazo **haihusiki** na uundaji wa maneno katika Lugha?
A. Kutofautisha uchumi na teknolojia katikajamii
B. Kukuza lugha katika jamii inayohusika
C. Kukidhi mahitaji ya mawasiliano
D. Kuibuka kwa mambo mapya katika jamii
E. Kuwa na msamiati wa kutosha katika lugha

x. Ni hatua inayofuata baada ya kipengere cha mwisho wa barua katika uandishi wa barua rasmi.
A. Jina la mwandishi
B. Cheo cha mwandishi
C. Saini ya mwandishi
D. Salamu za maagano
E. Jina la ofisi na jina la mwandishi

2. Oanisha fasili za tungo zilizopo katika **Orodha A** na dhana yake iliyopo katika **Orodha B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chako cha kujibia.

| **Orodha A** | | **Orodha B** |
|---|---|---|
| i. | Sehemu ya kiarifu inayokaliwa na nomino | A. Kirai |
| ii. | Neno au mpangilio wa maneno wenye neon kuu moja | B. Kishazi tegemezi |
| iii. | Sehemu ya kiarifu inayokaliwa na kielezi | C. Chagizo |
| iv. | Huundwa na vitenzi vyenye viambishi vya o-rejeshi | D. Shamirisho |
| v. | Ni kikubwa kuliko kirai lakini kidogo kuliko sentensi | E. Kishazi |
| vi. | "Mwanafunzi ambaye hakufika jana, asimame". Ni mfano wa sentensi…………………….. | F. Kiraikielezi |
| | | G. Sentensi changamano |
| | | H. Prediketa |
| | | I. Sentensi amabatano |
| | | J. kijalizo |

SEHEMU B (**alama 54**)Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Kwa kutumia mifano taja vipashio sita vya kiima
4. a)Eleza dhima ya kiambishi **"ni"** kilichopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:
   i. Ali<u>ni</u>saidia
   ii. Wajumbe wapo mkutano<u>ni</u>
   iii. Yeye <u>ni</u> mvivu
   iv. <u>N</u>inakulaumu

b) Bainisha aina za maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:
i. Kucheza <u>kwao</u> sikupendi tena.
ii. Mwanafunzi hodari hufaulu <u>mara kwa mara.</u>
iii. <u>Hiviataandika</u> barua mapema?.
iv.Nilipolilipua likalipuka <u>lipu!.</u>
v.Mwalimu anafundisha <u>darasani.</u>

5.a)Sentensi zifuatazo zina makosa ya kisarufi, ziandike upya kwa usahihi:
i. Huyu hapendi ugomvi.
ii. Mafanikio alidondoka pale wakati anakimbia.
iii. Mtoto angepelekwa hospitalini mapema angelipona.
iv.Mzee Peko alichinja mbuzi zake zote.

b) kwa kutumia mifano, andika miundo minne ya sentensi shurutia.



Scanned with CamScanner

6. Kijiji chenu cha Songambele kimeanzisha mradi wa kilimo cha umwagiliaji. Wewe kama afisa manunuzi wa mradi, andika barua katika kampuni ya Sungura inayojihusisha na uuzaji wa pembejeo za kilimo ukikiri kupokea bidhaa zitakazotumika katika kuendesha mradi. Jina lako liwe Bisheni Mtafunguliwa.
7. Kwa kutumia mifano kutoka katika riwaya ya Takadini na Watoto wa Mama Ntilie, kwa kifupi ukitumia hoja nne; mbili kutoka kila riwaya, eleza ni jinsi gani mwanaume ameonekana kuwa kikwazo cha maendeleo katika jamii. Tumia mzee Lomolomo na MzeeMakwati.
8. Soma beti zifuatazo za shairi la kimapokeo kasha jibu maswali yanayofuata.

1. *Tuitafute elimu, vitabu vyote vyasema,*
*Ni kitu kilo muhimu, kwa maisha yako mema,*
*Tuipate na idumu, ijenge yalo hekima,*
*Elimu dira sahihi, ongoza yetu maisha.*

2. *Elimu kwetu ni mali, uishike ninasema,*
*Haitaki ukatili, yakutaka uwe mwema,*
*Maisha kuyakabili, kuyafanya yawe mema,*
*Elimu dira sahihi, ongoza yetu maisha.*

**MASWALI;**

a) Bainisha ukwapi na utao wa mstari wa tatu wa ubeti wa pili.
b) Taja tamathali mbili za semi kwa mifano kutoka katika shairi ulilosoma.
c) Mwandishi wa shairi hili anazungumzia nafsi ipi? Thibitisha jibu lako kwa mifano miwili kutoka shairi ulilosoma.
d) Elimu humpatia mtu fedha kutokana na taaluma aliyonayo lakini kuna watu wana fedha nyingi ila hawana elimu. Kwa mujibu wa shairi hili unadhani watu hao wanakosa kitu gani cha msingi? Eleza kwa hoja moja.

## SEHEMU C. (ALAMA 30)

Jibu maswali **mawili (02)** katika sehemu hii.Swali la **tisa (09)** ni la lazima na kila swali lina alama **kumi na tano (15).**

**ORODHA YA VITABU**

**USHAIRI**
- **Wasakatonge.** - **MS Khatibu (DUP)**
- **MalengaWapya** - **TAKILUKI (DUP)**
- **MashairiyaChekacheka** - **T. A. Mvungi (EP &D. LTD)**

**RIWAYA**
- **Takadini.** - **Ben J. Hanson (MBS)**
- **Watotowa Mama N'tilie.** - **E. Mbogo (H.P)**
- **Joka la Mdimu.** - **A.J. Safari (H.P)**

**TAMTHILIYA**
- **Orodha.** - **Steve Reynolds (MA)**
- **Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe.** - **E. Semzaba (ESC)**
- **Kilio Chetu.** - **Medical Aid Foundation (FPH)**

9. Washairi ni waatalamu wazuri na waliobobea katika kutumia jazanda zinazotoa ujumbe kwa jamii. Tumia jazanda tatu kwa kila diwani mbili ulizosoma.

10. "Mwanamke ni mtu mwenye huruma na fadhira." Thibitisha hoja hiyo kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu kutoka katika vitabu viwili vya riwaya ulivyosoma.

11. "Msanii wa kazi ya fasihi huwa haoti akiwa anatayarisha kazi yake" kwa kutumia hoja tatu kutoka tamthilia mbili ulizosoma thibitisha kauli hii.( hoja tatu kwa kila kitabu)



Scanned with CamScanner